035713655

KENYA NATIONAL PREDICTION TESTS

# KCPE

516004

## KISWAHILI
## SEHEMU YA KWANZA
## LUGHA

**Muda: Saa 1 dakika 40**

**MAAGIZO KWA WATAHINIWA**
**SOMA MAAGIZO YAFUATAYO KWA MAKINI.**

1. Umepewa kijitabu hiki cha maswali na karatasi ya kujibia. Kijitabu hiki kina maswali 50.
2. Ukisha chagua jibu lako lionyeshe katika **KARATASI YA MAJIBU** na wala siyo katika kijitabu hiki cha maswali.

**JINSI YA KUTUMIA KARATASI YA MAJIBU**

3. Tumia penseli ya kawaida.
4. Hakikisha ya kwamba yafuatayo yameandikwa katika karatasi ya majibu:

**NAMBA YAKO YA MTIHANI**
**JINA LAKO**
**JINA LA SHULE YAKO**

5. Kwa kuchora kistari katika visanduku vyenye namba zinazokuhusu, onyesha namba yako kamili ya mtihani (yaani namba ya shule, na zile namba tatu za mtahiniwa) katika sehemu iliyotengwa mwanzo wa karatasi ya majibu.
6. Usitie alama zozote nje ya visanduku.
7. Iweke safi karatasi yako ya majibu na usiikunje.
8. Kwa kila swali 1-50 umepewa majibu manne. Majibu hayo yameonyeshwa kwa herufi A, B, C, D. Ni jibu MOJA tu kati ya hayo manne ambalo ni sahihi. Chagua jibu hilo.
9. Kwenye karatasi ya majibu, jibu sahihi lionyeshwe kwa kuchora kistari katika kisanduku chenye herufi uliyochagua kuwa ndilo jibu.

**Mfano:**

**Katika kijitabu cha maswali:**

**22.** Barua ya kuomba kazi huitwa
   A. waraka
   B. barua maalum
   C. barua ya kiofisi
   D. Barua rasmi

Jibu sahihi ni **D**

**Katika karatasi ya majibu:**

**2.** [A] [B] [C] [D] **12.** [A] [B] [C] [D] **22.** [A] [B] [C] [D] **32.** [A] [B] [C] [D] **42.** [A] [B] [C] [D]

Katika visanduku vinavyoonyesha majibu ya swali namba **22**, kisanduku chenye herufi **D** ndicho kilichochorwa kistari.

10. Chora kistari chako vizuri. Kistari chako kiwe cheusi na kisijitokeze nje ya kisanduku.
11. Kwa kila swali, chora kistari katika kisanduku **kimoja tu** kati ya visanduku vinne ulivyopewa.

**Kijitabu hiki cha maswali kina kurasa 7 zilizopigwa chapa.**

906504

© Mtihani Bora

**GEUZA UKURASA**

**Soma vifungu vifuatavyo. Vina nafasi 1 mpaka 15. Kwa kila nafasi umepewa majibu manne. Chagua jibu lifaalo zaidi kati ya yale uliyopewa.**

Juzi ___1___ katika ofisi ya gavana wa jimbo ___2___, nilifurahia hadhi mpya ya lugha ya Kiswahili. Hapo ndipo niliposadiki kweli kuwa nchini mwetu mna mwamko mpya. Ukweli ni kuwa katiba mpya___3___ Kiswahili na hivi leo ___4___ hapo awali Kiswahili kinatumiwa ___5___ kiingereza kama lugha ramsi. Hebu tafakari gavana alipoingia aliniamkua, ___6___ nami nikamjibu,___7___. Nilishangaa ___8___asubuhi hiyo nilitarajia atumie kiingereza jinsi alivyozoea.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 1. | A. nilivyoingia | B. nilipoingia | C. niliyoingia | D. nilioingia |
| 2. | A. letu | B. yetu | C. chetu | D. zetu |
| 3. | A. imekieneza | B. imekitia fora | C. imekitweza | D. imekikuza |
| 4. | A. kinyume na | B. kinyume cha | C. kando ya | D. Kando na |
| 5. | A. sawia na | B. mbali na | C. miongoni mwa | D. kati ya |
| 6. | A. makiwa | B. buriani | C. masalkeri | D. sabalkheri |
| 7. | A. tunayo | B. buriani dawa | C. aheri | D. marahaba |
| 8. | A. taraa | B. maadamu | C. wala | D. ingawa |

Leo hii unaweza kutuma ombi la kazi___9___ kutumia Kiswahili bila kuonekana kama ___10___. Ni vyema ijulikane kuwa Kiswahili ___11___ lugha unganishi tu hapa nchini ___12___ bali pia katika ukanda ___13___ wa Afrika ya Mashariki. Wengi tumefaidi kutokana na Kiswahili na kama wasemavyo wahenga ___14___. Leo kazi kubwa ya Kiswahili ni ___15___ wakazi wote wa Afrika ya Mashariki.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 9. | A. na | B. ya | C. za | D. kwa |
| 10. | A. unajidumisha | B. unajidunisha | C. unakidumisha | D. unakihimiza |
| 11. | A. kimekuwa | B. imekuwa | C. hakijakuwa | D. halijakuwa |
| 12. | A. mwetu | B. petu | C. yetu | D. kwetu |
| 13. | A. mzima | B. nzima | C. zima | D. lizima |

14. A. akufaaye kwa dhiki ndiye rafiki — B. mkulima mmoja walaji wengi — C. aisifuye mvua imemnyea — D. penye nia pana njia

15. A. kuwadumisha na kuwajenga — B. kuwastawisha na kuwalenga — C. kuwahamasisha na kuwalenga — D. kuwatambulisha na kuwaunganisha

**Kutoka swali 16 mpaka 30 chagua jibu sahihi.**

16. Chagua sentensi iliyotumia **-ki-** ya udogo.
   A. Hata akienda juu atashuka tu atupate hapa hapa.
   B. Kikoba chake hakiwezi kutoshea vitabu hivyo.
   C. Lugha ya kichina ni ngumu, haizungumziki kwa urahisi.
   D. Kisu kitanolewa ili kiweze kukatia nyama

17. Chagua methali ambazo zina maana sawa.
   *(i) Usipoziba ufa utajenga ukuta*
   *(ii) Vyote viowevu si maji*
   *(iii) Samaki mkunje angali mbichi*
   *(iv) Usidharau kiserema chalima kuliko jembe*
   A. ii na iv
   B. i na ii
   C. i na iii
   D. iii na iv

18. Wao walimsifu kiongozi wao aliyetoka ng'ambo. Tambua maneno yaliyopigiwa mistari.
   A. Nomino, kivumishi, nomino
   B. Kiwakilishi, kivumishi, kielezi
   C. Nomino, kiwakilishi, kielezi
   D. Kivumishi, kielezi, nomino

19. Chagua sentensi iliyonyambuliwa katika kauli ya kutendesha kwa usahihi.
   A. Askari walimkimbisha mwizi kwa hasira.
   B. Waliamua kututembesha katika bustani ya Uhuru.
   C. Jaji alimtoza mhalifu faini ya shilingi milioni sita.
   D. Umati wa watu ulidumiza amani katika mkutano wa kisiasa.

20. Chagua sentensi iliyo katika hali timilifu.
   A. Mwanafunzi aliandika insha kisha akampelekea mwalimu asahihishe.
   B. Timu hiyo haijacheza jinsi nilivyotarajia
   C. Paka huwanyonyesha wanawe msimu wa baridi kali.
   D. Mwanafunzi asomaye na kujifunza mengi hufaulu kila wakati.

21. Chagua kundi lenye vihusishi pekee.
   A. Zuri, ubavuni pa, katika, kwenye
   B. Ubavuni pa, katika, kwenye
   C. Vyema, vibaya, polepole, haraka
   D. Ingawa, seuze, laiti, bali

22. Ni nini umoja wa:
   Kucha za watoto wakorofi zilikatwa zilipokuwa ndefu.
   A. Makucha ya mtoto korofi yalikatwa yalipokuwa marefu.
   B. Kucha ya mtoto mkorofi ulikatwa ulipokuwa mrefu.
   C. Ukucha wa mtoto mkorofi ulikatwa ulipokuwa mrefu.
   D. Kucha za mtoto korofi zilikatwa zilipokuwa ndefu.

23. Chagua sentensi iliyoakifishwa ipasavyo.
   A. Ebo, huoni huyo hafanani na dada yako.
   B. Juni-mwezi-huu tumepangiwa sherehe ya kukata na shoka.

C. Amos (anayefunza somo la Mlahaka) ameteuliwa kuwa kaimu mwalimu mkuu katika shule yetu.

D. Ukienda dukani, hakikisha umenunua vitu vifuatavyo sukari, chumvi, mafuta na mboga.

**24. Andika wa wingi:**

Baraza langu huongozwa na nahodha bahiri

A. Mabaraza yangu huongozwa na nahodha bahili.

B. Mabaraza yetu huongozwa na nahodha mabahili.

C. Baraza zetu huongozwa na manahodha mabahili.

D. Mabaraza yetu huongozwa na manahodha bahili.

25. Ni sentensi gani sahihi?

A. Lau abiria akikosa nauli hawezi kusafiri.

B. Lau ungemtembelea mapema angekutatulia shida hiyo.

C. Amebaki lau hakuwa na mpango wa kusafiri.

D. Nipe lau shilingi mia moja ninunue chipsi.

26. **Kanusha:** Simu ambayo ilinunuliwa iligharimu pesa nyingi.

A. Simu iliyonunuliwa haijagharimu pesa nyingi.

B. Simu iliyonunuliwa haigharimu pesa nyingi.

C. Simu ambayo haikununuliwa haikugharimu pesa nyingi.

D. Simu ambayo ilinunuliwa haikugharimu pesa nyingi

**27.** Kifaa cha ufundi kinachotumiwa kutolea au kuingizia misumari ya skrubu huitwaje?

A. Patasi

B. Jiriwa

C. Keekee

D. Bisibisi

**28.** Chagua orodha yenye viungo vya nje ya mwili.

A. Ufizi, nyonga, ubongo

B. Mboni, ini, moyo

C. Nyonga, ndewe, kwapa, kidole

D. Kionjamchuzi, kwapa, ini

**29.** Chagua sentensi yenye 'karibu' ya kihusishi cha mahali.

A. Mwanafunzi amesimama karibu na uwanja.

B. Mlevi huo karibu aanguke mtoni.

C. Karibu tucheze ngoma.

D. Mama karibu kukosa matwana

**30.** Tegua kitendawili kifuatacho.

Hauna jua hauna mvua wakati wowote humea

A. Mti

B. Unywele

C. Maradhi

D. Msitu

**Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 31 - 40.**

Je, wewe unaitumia lugha gani? Kila mmoja ana lugha yake anayoienzi. Wengi wa Wakenya wanaienzi lugha ya Kiswahili. Tangu iidhinishwe katika katiba ya Kenya takribani miaka kumi na mmoja iliyopita kama lugha rasmi wakereketwa wana matumaini kama tai kuwa Kiswahili kitawalisha kikoa wote. Licha ya matumaini haya yenye nia nzuri, Kiswahili bado kingali kinakabiliwa na changamoto tele.

Shida ya kwanza ni kuwa kwa sasa hakuna sheria bungeni ya kuhakikisha kuwa lugha hii inapewa nafasi kulingana na hadhi yake mpya iliyotunukiwa. Kwa mfano hapajatolewa tamko rasmi kuhusu adhabu watakazopewa watu ambao hawakitumii inavyostahiki. Aidha hapajabainishwa haki watakazofaidi wale wanaokitumia ipasavyo au watakazohiniwa wanaokaidi kanuni zinazoenda na hadhi ya lugha hii rasmi na ambayo pia ni lugha ya taifa.

Ukweli usiopingika ni kuwa katiba imependekeza katika viambatisho vyake vyombo ambavyo ni miega ya kutekeleza vipengele mbalimbali, lakini haijashauri uundaji wa baraza na taasisi ya kuikuza na kuiendeleza lugha ya Kiswahili. Hivyo sasa maendeleo ya lugha hii yanatokea tu kwa kudura za Mola na juhudi za wadau akali. Hii ni dhihirisho tosha kuwa kuna kibarua cha ziada ambacho kinatakikana.

Kutokana na niliyokuelezea, ni wazi basi wananchi wengi wanakisifu Kiswahili kimdomo tu barazani lakini wakiwa upenuni wanakikashifu Kiswahili, si siri wakenya wengi wanakidharau Kiswahili. Hebu watazame wengi iwe shuleni au umatini. Wanachukulia kuzungumza Kiingereza kama ishara ya ustaarabu. Kiswahili kinahusishwa na ulimbukeni au ushamba. Licha ya kuwa Kiswahili kimewalea watu wengi, ambao kwa kweli wamenufaika si haba, bado baadhi yao hawaienzi. Watu kama hawa hufedheheka wao au watu wengine wanapokiboronga Kiingereza lakini huona ni jambo la kawaida Kiswahili kinapobambanywa. Hebu fikiria kuna wengine hawawezi kusoma makala ya Kiswahili mahali wazi.

Hatua ya serikali kuwa Kiswahili kifunzwe na kutahiniwa katika shule ni hatua za kibinafsi na hasa za kimataifa wanakosomea watoto wa walalaheri wenye vyeo na vyeo. Huko ng'ambo lugha ya taifa na lugha ya kwanza rasmi ya nchi haifunzwi na inapofunzwa ni kwa kulipwa tu. Hili linachangia katika kuharibu lugha na tunu za taifa kama usawa, uzalendo, umoja na udugu.

Shangaa kisha ushangae tena hata baadhi ya vyuo vikuu vinaegemea sana mafunzo ya kisayansi. Ni vizuri ieleweke kuwa mataifa yaliyoendeelea huweza kuafikia maendeleo makubwa kupitia vyuo vikuu vya mataifa haya ambayo hutumia lugha zao za taifa kufunzia. Hapa nchini, badala ya kuchukua mwelekeo huo, baadhi ya vyuo vikuu vinaona fahari kuvianzisha vituo na taasisi za lugha kama kichina au kijapani kuliko asasi za Kiwahili. Waelewe ni vibaya kuacha lugha yetu ya Kiswahili na kuzikumbatia lugha za ugenini.

Tukiangalia shule zetu za msingi na za upili, matokeo ya somo la Kiswahili yamekuwa yakidorora kila uchao. Lawama za hali hii ya kusikitisha zimekuwa zikielekezwa kwa 'sheng' kama adui mkubwa wa Kiswahili sanifu. Wengi wanadai kuwa wanafunzi wanatawaliwa na kilugha hiki kiasi cha kupuuza Kiswahili sanifu. Ajabu ni kuwa hata walimu hawajasazwa. Hata wao wanatumia 'sheng'. Hatusemi ni makosa walimu hawa wanafanya lakini ni vizuri wajue mahali na wakati wa kutumia sheng.

Licha ya yote hayo, ni jambo la kutia moyo kuona kuwa kiswahili kinatumiwa kupeperushia matangazo ya taarifa za habari. Ni jambo la kawaida siku hizi kuona mijadala mikali juu ya mada anuwai kwenye idhaa na vituo vya televesheni kwa Kiswahili. Lile linalosikitisha hata hivyo ni kiwango cha chini cha usanifu wa lugha inayotumiwa na wanaochangia. Kwa kawaida wao hufanya makosa mengi ya ngeli, msamiati hata aina za maneno.

31. Taja tamathali mbili za lugha ambazo zinajitokeza katika kauli hii Wana matumaini kama tai kuwa Kiswahili kitawalisha kikoa wote.
A. Tashbihi, nahau
B. Tashbihi, tashhisi
C. Nahau, chuku
D. Kinaya, ishara

32. Kulingana na aya ya kwanza,
A. ni miaka kumi na mmoja imepita tangu Kiswahili kiidhinishwe kuwa lugha rasmi
B. ni chini ya miaka kumi na mmoja sasa tangu Kiswahili kiidhinishwe kama lugha rasmi.
C. ni zaidi ya miaka kumi na mmoja sasa tangu Kiswahili kiidhinishwe kama lugha rasmi
D. ni karibu miaka kumi na mmoja sasa tangu Kiswahili kiidhinishwe kama lugha rasmi.

33. Kauli hii ina maana gani?
..... ni hatua za kibinafsi na kimataifa wanakosomea watoto wa walalaheri wenye vyeo na vyeo.
A. Shule zote za kibinafsi na kimataifa ni za matajiri.
B. Shule huweza kuonyesha uwezo wa kiuchumi wa watu.
C. Hakuna maskini wanaomudu kuwapeleka watoto wao katika shule za kibinafsi.
D. Shule za kibinafsi ni bora kuliko zile za umma.

34. Kulingana na aya ya pili, ni kweli kusema kuwa
A. umaarufu wa lugha ya kiswahili unazidi kufifia kutokana na changamoto tele.
B. kura ya maoni ilihitajika bungeni ili kuunda sheria za kuhakikisha kuwa lugha hii imepewa hadhi yake mpya iliyotunukiwa.
C. baada ya Kiswahili kukwezwa hadhi palikuwa na haja ya kubadilisha sheria za nchi.
D. wengi wa wakenya wanajivunia kutumia lugha ya Kiswhaili katika makongamano ya taifa.

35. Waswahili husema kuwa 'ivushayo ni mbovu'. Ukweli wa methali hii unadhihirika pale
A. baadhi ya wale ambao hawaithamini lugha ya Kiswahili wamefaidi lugha hii
B. hakuna msomi hata mmoja anayeenzi usomaji wa makala yaliyoandikwa kwa Kiswahili.
C. wengi wanaienzi lugha ya Kiingereza kuliko ya Kiswahili
D. maendeleo ya nchi yetu yamegandamiwa na Kiswahili.

36. Kifungu hiki kimetubainishia kuwa vyuo vikuu vya hapa nchini
A. havifunzi mafunzo ya lugha yoyote ile
B. havithamini elimu ya lugha hata kidogo
C. vinathamini sana lugha za kigeni
D. vinathamini sana lugha ya Kiswahili.

37. Kifungu hiki kimeonyesha wazi kuwa
A. si makosa kutumia 'sheng'.
B. 'sheng' ni lugha haramu kabisa
C. 'sheng' inafaa kufanywa lugha ya taifa
D. ni walimu pekee wanaotumia lugha ya 'sheng'

38. Waelewa ni vibaya kuacha lugha yetu ya Kiswahili na kuzikumbatia lugha za ugenini. Ni methali gani inayojumuisha, ujumbe wa kauli hii?
A. Mgeni njoo mwenyeji apone
B. Mwacha asili ni mtumwa
C. Kazi mbaya si mchezo mwema
D. Mavi ya kale hayanuki

39. Wadau akali ni
A. watu wachache wenye maslahi ya elimu.
B. watu wachache wasiopenda elimu
C. watu wakali wenye maslahi ya elimu
D. watu wakali wasio na maslahi ya elimu

40. Kichwa kifaacho makala haya ni.
A. Matumizi ya lugha ya kiswahili
B. Changamoto zinazokabili lugha ya Kiswahili.
C. Manufaa ya lugha ya Kiswahili
D. Lugha ya taifa

**Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 41 - 50.**

Kutokana na uchovu niliokuwa nao, nilienda moja kwa moja hadi kulaza mbavu. Nilikuwa nimeanza kulitamwa joto la blanketi niliposikia yowe kali. Sikuchukulia kwa uzito. Kwanza nilituhumu zilikuwa kelele za walevi wakitoka magengeni. Niliamua kusikiza kwa makini. Sauti ya pekee niliyosikia ilikuwa ya mbu ambaye alikuwa akizurura akisaka pale ambapo angeuzika usinge wake kwenye mwili wangu. Moyo nao ulinidunda kama ngoma.

Baada ya kuona hakukuwa na la mno, niliamua kujizika tena katika blanketi langu. Nao ule ukelele ulisikika tena. Hapo ndipo nilichomoka nje kama mshale. Nilichukua kurunzi iliyokuwa mbalamwezi. Nilielekea mlangoni. Kumbukumbu ya masaibu yaliyowasibu wanakijiji yalijiradidi akilini. Hapo ndipo niliamua kushirikiana na wenzangu.

Kwa utaratibu, niliufungua mlango. Nilichelea kutoa kelele zozote ambazo huenda zingekitia kitumbua mchanga. Nilitoka na kuutia mlango komeo kwa nje. Niligutukia kuwa hapo nje palikuwa na majani makavu yaliyokuwa yamepukutika kutoka mitini. Niliamua kutembea kwa ncha za miguu. Nilitokea pale watu walikuwa wamesimama.

Tukiwa tumeduwaa na yale yaliyotukia, usiahi ule ulitokea tena. Mara hii ulisikika waziwazi kama mwangwi wa sauti. Sote tulishika njia kuelekea upande huo. Tulipofika kwenye njia-panda tulijigawa katika mafungu mawili. Niliamua kuwa katika kundi la kwanza. Tulipitia kwenye mzoga wa mnyama. Harufu ya uozo ilitapakaa kila mahali ikatupenya kwenye mianzi ya pua na hata kutukirihi. Harufu haikutusumbua maadamu tulitaka kuondoa dari ili kuezeka paa.

Tulikuwa gizani. Mara tulishtuliwa na miterekenyo iliyokuwa mbele yetu. Tulikaa tutwe ya mtu. Hakuna aliyesema chochote ila kila mtu aliweza kusikia mipumuo ya wenzake. Kwa kauli moja tuliamua kujibonza kwenye vichaka vilivyokuwa kando ya njia. Kwa muda wa kuukwea mnazi na kushuka tuliona pandikizi la mtu ambalo lilikuwa likivuta mtu. Ule unyende ulitoka lakini kwa shida. Kila mtu alijiandaa vilivyo kwa kuwa wakati ambao tulikuwa tumeusubiri ulikuwa umewaida. Jitu lile lilipumua kama mnyama aliyekuwa akiumwa. Lilipokaribia, ilikuwa wazi kwamba binadamu aliyekuwa amebebwa ndiye aliyekuwa akiutoa unyende ule.

Liliponifikia, nililitega nalo likaanguka pu! Nao wenzangu walitokeza bila kukawia. Yule msichana aliyekuwa akitoa ukelele alikurupuka mbio kabla ya kutegwa na mwenzangu na kuanguka. Alieleza kuwa ametekwa nyara na mwanamume yule akiwa na lengo la kumnajisi. Watu walipandwa na hamaki na kuhisi kulipasua lile jitu katili. Mimi binafsi licha ya kujua ningeonekana msaliti na wenzangu nilikataa ombi hilo. Niliwaambia tusifanye uamuzi wa papare ili tuweze kukata mzizi wa ubakaji. Lengo langu lilikuwa jitu hilo liwataje washirika wake ili tuwatambue wote na kuweza kufikishwa mahakamani na kutumikia kifungo chao.

Juhudi zangu hazikuambulia patupu. Wenzangu walikubaliana nami. Tulimfunga mwanamume yule kwa kamba na kumweka kizuizini. Siku iliyofuata tulimfukisha mahakamani ilipoamuriwa awe mahabusu

41. Msimulizi alidhani kelele
A. zilitoka kwa walevi waliokuwa wameenda kulewa
B. zilikuwa za watoto waliokuwa wakicheza nje
C. zilikuwa ni za bibi na bwana waliokuwa wakipigana
D. zilikuwa za waehezaji waliokuwa uwanjani

42. Kulingana na aya ya kwanza msimulizi alikuwa katika hatari ya kuambukizwa ugonjwa gani?
A. Malale
B. Malaria
C. Ukimwi
D. Pepopunda

43. Kwa mujibu wa kifungu
A. msimulizi alikuwa na woga wa kumenyama na waleta fujo katika eneo lao.
B. matatizo ya wanakijiji kuhusu usalama wao yalimchochea msimulizi kuwasaidia kutafuta chanzo cha ukelele.
C. msimulizi aliamrishwa kuamka na raia waliotaka ushirikiano wa wote.
D. msimulizi alikuwa pekee yake katika shida hiyo ya kuvamiwa.

44. <u>Nilichukuwa kurunzi iliyokuwa mbalamwezi</u>. Hii ni tamathali gani ya lugha?
A. Chuku
B. Tashbihi
C. Istiara
D. Nidaa

45. Makao ya msimulizi yalikuwa
A. yamejitenga na mengine na yalionekana wazi.
B. yamezingirwa na miti iliyoangusha majani makavu.
C. jangwani na ndiyo maana alieweza kuusikiliza usiahi vizuri.
D. yameezekwa kwa makuti si kwa mabati.

46. <u>Harufu haikutusumbua maadamu tulitaka kuondoa dari ili kuezeka paa.</u> Kauli hii ina maana ya
A. watu waliumizwa sana na harufu ya kukirihi iliyotoka katika mzoga
B. watu hawakujali hatari yoyote iliyowe kabili kwa kuwa walikuwa wamejihami
C. wote walitakiwa kuondoa woga waliokuwa nao iwapo walidhaminia kufaulu
D. harufu mbaya haikuwajalisha kuliko hofu iliyotokana na ukovu na usalama

47. <u>Tulikaa tutwe ya mtu.</u> Yaani
A. kuwa tayari kwa chochote
B. kushangaa sana
C. kunyamaza bila kusema chochote
D. kuogopa hali mbaya

48. Jitu lilikuwa na lengo la kutekeleza maovu yapi mawili?
A. Utekaji nyara, ubakaji
B. Uuaji, unajisi
C. Unajisi, ulanguzi wa dawa za kulevya
D. Utekaji nyara, ulanguzi

49. Mahabusu kwa mujibu wa kifungu ni
A. mahali ambapo watukumiwa wa kesi hufungiwa.
B. mfungwa angojeaye kesi yake isikiilizwe
C. anayeamua kesi mahakamani
D. pesa zinazotolewa mahakamani ili mshukiwa aachiliwe huru

50. Utaratibu gani ungefuatwa kisheria kwa jitu?
A. Mahakamani - Kizuizini- jela- rumande
B. Rumande- kortini- kizuizini- jela
C. Jela - kizuizini - mahakamani - rumande
D. Kizuizini- kortini- rumande - jela

***Malizia insha yako kwa***

.............................. baada ya hayo alijilaumu kwa kutomkanya mwanawe mapema. Hakika majuto ni mjukuu.